



“Bwana asipoijenga nyumba, Waijengao wafanya kazi bure.”
(Zaburi 127:1)

SALA kwa mujibu wa SHABAHA ZA LAUDATO SI' kwa Jamii zinazojiunga na Jukwaa Tendaji la Laudato Si'

Jumapili - Ombi kwa Parokia na Dayosisi



Mungu Muumba, tunazionbea parokia na dayosisi zetu, kwamba zitakuwa makini kwa Kilio cha Dunia na kukuza nishati safi, hewa safi na maji kwa wote, kuvilinda vyote vilvyoumbwa na Mungu, na bioanuwai na hasa hali ya hewa. Na tuweze kugundua upya wito wetu kama waangalizi wa dunia ; makao yetu na pia wa mtu na mwenzake.

Jumanne - Ombi kwa ajili ya Uchumi



Mungu Mpaji, tusaidie kuleta “pamoja nyanja tofauti za maarifa, zikiwemo za kiuchumi,” na kukuza “mifumo mipy ya maendeleo muhimu.” Na tuweze kujituma zaidi kwa kwa dhana mpya ya kiuchumi katika huduma kwa wote.,” pasipo kumsaza yejote.

Alhamisi - Ombi kwa Taasisi za Kielimu



Mungu wa Maarifa na Maadili, tuwezeshe “kukua kwa ushikamano, uwajibikaji na huduma za huruma.” Na uziwezeshe shule zetu na vyuo kukuza, hasa *elimu* ambayo inaweza kurejesha, “ upatanifu mionganoni mwetu na Mungu, na wenzetu wengine, maumbile na viumbe wote walio hai.”

Jumatatu - Ombi kwa familia



Mpenzi wa wanyonge, tunazionbea familia zote ili kwamba ziwe “ mahali ambapo maisha - zawadi kutoka kwa Mungu - yanaweza kulakiwa na kulindwa.” Na ziweze hasa kuwa makini kwa Kilio cha Wanyonge na kujituma kwa maisha kamilifu kwa wote, hususan kwa walio katika hatari za kudhuriwa zaidi, na kwa wenzetu walitolekelezwa katika familia hii yetu sote.



Jumatano - Ombi kwa hospitali zetu



Mungu Mtunza, tunazionbea taasisi zetu, hasa hospitali na vituo vyetu vya afya, ili kwamba vikue katika uwezo wavyo wa kuhudumu. Na tuweze sote kuelewa na kuthamini namna matendo kamilifu na mitindo sahali ya kimaisha inavyowezesha wengine kuishi na kunawiri.

Ijumaa - Ombi kwa mashirika



Mungu wa Utatu Mtakatifu, yasaide mashirika, Asasi Zisizo za Kiserikali, vituo vya mawasiliano, na makundi yote yafanyayo amali za wema kwa wote, kuvuvumua *kiroho* ushikamano wa kilimwengu unaotokana na fumbo lako, muunganiko wa jumuia ya mapendo.

Jumamosi - Ombi kwa mashirika ya kidini



Mungu wa Ushirika, tuwezeshe kuwa *jamii* za kimatendo na yenye kutetea dunia na wanyonge. Yaweeshe mashirika yetu ya kidini, hasa kuwa, viongozi, manabii wa huduma katika utunzaji wa ulimwengu; makao yetu, na kwa wote wenye hadhi ya chini mionganoni mwetu.

